

- vii. **"a e i o u"** hizi ni katika lugha ya kiswahili.
 A. irabu B. Silabi. C. Konsonati. D. Sentensi. []
- viii. ni neno kuanzia moja na kuendelea yanayotoa ujumbe kamili.
 A. Herufi. B. Sentensi. C. Silabi. D. Konsonati. []
- ix. "Tulicheza ngoma na kuimba usiku kucha" katika sentensi hii watenda ni nafsi ipi?
 A. Ya tatu wingi. B. Ya pili wingi. C. Ya kwanza wingi. D. Ya kwanza umoja []
- x. Ni neno lipi kati ya haya yafuatayo ni **tofauti** na mengine?
 A. Sahibu. B. Ajuza. C. Mwandani. D. Mwenzi. []

2. Oanisha nahau zilizopo katika ORODHA A na maana zake zilizopo katika ORODHA B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi maana sahihi ya kiswahili.

ORODHA A	ORODHA B
i. Ameoa	A. Ana mkono mrefu
ii. Shauri yako	B. Kula mlungula
iii. Ni mwizi	C. Mtu mwenye ndimi mbili
iv. Kula rushwa	D. Utalijua jiji
v. Kigeugeu	E. Kapata jiko
	F. Kula pilau
	G. Na kuolewa

ORODHA A	i	ii	iii	iv	v
ORODHA B					

SEHEMU B (Alama 70)

Jibu maswali yote

3. Sentensi zifuatazo zinamakosa kisarufi, pigia mstari kosa lililopo kisha rekebisha sentensi hiyo.

- a) Sisi wote tunapaswa kwenda shuleni _____
- b) Yuko hapa _____
- c) Ni budi ufanye kazi _____
- d) Maneno hayo hutumika na watu wengi _____

e) Nyumba imeingia nyoka

f) Yule ndio aliyekuja

g) Zamira kuu ni rushwa

h) Nililipatiapo jawabu

i) Mbuzi zetu ni nyingi

j) Wale vijana wanapenda pombe

4. Unda maneno yenye vitamkwa vifuatavyo:

i. Konsonati + irabu + konsonati + irabu =

ii. Konsonati + konsonati + irabu =

iii. Irabu + irabu + konsonati + irabu =

iv. Konsonati + irabu + irabu =

v. Irabu + irabu =

5. Bainisha aina za maneno zilizokolezwa wino

Mfano: **Asha** anapenda kusali

Asha ni nomino

a) Baba anapenda kujua **ndoto** zangu

b) Wanafunzi **wote** wanapenda kula wali

c) Hiki chenyewe ni **kifupi**

d) Watafika kesho **kwa ajili ya** mkutano

e) Sisi tunapenda nguo **za michezo**

f) Aliahidi kumpenda **daima**

g) **Kucheza** kwake kunafurahisha

h) Sisi **tungali** wafupi

i) Walikula **japokuwa** hawakushiba

j) **Huyu** ndiye aliyenitorosha

6. Tunga sentensi kwa kutumia vipashio vifuatavyo

a) W + T+ N

b) N + V + T

c) W+V+Ts+T+E

d) N+V+Ts+Ts+ T+N

e) T + U + T +N

7. i) Nini maana ya kamusi?

ii) Samweli alikuwa anasoma habari alikuta msamiati "Handaki" akawa hajui maana yake.hivyo akaenda mezani kutafuta kitabu cha marejeleo ili aweze kutafuta maana ya neon hilo.je ni faida gani anaweza kuzipata samweli baada ya kusoma kitabu hicho (hoja nne)

a) _____

b) _____

c) _____

d) _____

8. Wewe ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza ambaye unalipenda somo la Kiswahili na unaliweza sana. Taja dhima ya lugha katika mawasiliano.

a) _____

b) _____

c) _____

d) _____

e) _____

9. Eleza maana ya istilahi zifuatazo:

a)Mawasiliano _____

b)Lugha _____

c)Lugha
fasaha _____

d)Kiimbo _____

e)Mkazo _____

SEHEMU C (Alama 15)

10. Kutokana na maarifa uliyopata darasani kuhusu fasihi, fafanaa dhana ya fasihi kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo;

a) Fanani ni nani katika kazi ya fasihi?

b) Unaelewa nini kuhusu hadhira wa fasihi?

c. Taja tofauti tano kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi.

FASIHI SIMULIZI	FASIHI ANDISHI
i.	i.
ii.	ii.
iii.	iii.
iv.	iv.
v.	v.